

Maswali

1. Nani aliyeitoa hadithi ya shilingi iliyopotea?
2. Mwanamke alikuwa na shilingi ngapi?
3. Mwanamke huyo alikuwa akifanya nini siku hiyo?
4. Kwa nini hakuwa mchangamfu?
5. Alifanya nini ili kupata shilingi iliyopotea?
6. Alipata wapi shilingi hiyo?
7. Aliwaambia nani kuwa amefurahi?
8. Ni wakati gani tunapotoka kutoka kwa Mungu?
9. Tunaweza kufanya nini ili Mungu atukubali tena?
10. Mungu husikiaje tunapomrudia?

Majibu

1. Yesu.
2. Kumi.
3. Alikuwa na shughuli ya kufagia nyumba na kupika.
4. Alipoteza moja wapo ya shilingi zake.
5. Alitafuta shilingi kwa kufagia nyumba akiinuwa taa.
6. Alipata mahali kulipokuwa na giza zaidi chumbani mwake.
7. Marafiki zake na majirani.
8. Tunapo fanya makosa.
9. Tumwambie Mungu atusamehe.
10. Mungu hufurahia.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

40 Shilingi iliyopotea

Marejeo

Luka 15:8—10

Kiini cha somo

Kuonyesha kuwa Mungu hufurahia tunapomwomba msamaha na kumrudia

Maneno maalum

1. Kufanya uovu + kupotea + kuomba msamaha + Mungu kuridhika + malaika
2. Mwanamke + shughuli + chakula + shilingi kumi
3. Shilingi + tisa pekee + moja ilipotea + kuhuzunika +kuambia marafiki
4. Alitafuta + ufagio + kufagia + kapata shilingi + furaha
5. Kufanya uovu + Mungu kuhuzunika + kuomba msamaha + Mungu kufurahia

40.1 Habari hii aliisema Yesu. Mara nyingi tunafanya mambo ambayo ni makosa. Ni sawa na kupotea asiwe na Mungu tena. Na tunapomba tena msamaha, jinsi inavyomfurahisha Mungu kutupata. Anafurahi sana akiwa pamoja na malaika zake mbinguni.

40.2 Siku moja asubuhi wakati jua lilipokuwa linaangaza sana, mwanamke alikuwa na kazi katika nyumba yake ndogo. Ilikuwa imezekwa kwa kuinuliwa sana paa zake.

Nyumba yake ilijengwa kwa mawe na tope na madirisha yake yalikuwa ni madogo kuweza kufanya ndani yake kuwa baridi wakati wa joto sana ilipofika mchana. Na ilifanya chumba kiwe na giza.

Mme na wana wake walikuwa wamekwenda kazini. Ndipo alipofagia na kufuta vumbi. Yule mwanamke alikuwa na shilingi kumi za fedha ambazo alizipenda sana. Alikuwa hajawahi kuwanazo tangu aolewe. Huenda alizifunga kamba pamoja na kuzivaa kama utepe usoni pake. Na mara nyingi aliacha kufanya kazi kwa muda ili tu aziangalie sarafu zake hizo ambazo ziling'aa sana.

Kisha baadaye, akaanza kutayarisha chakula cha mchana. Kwanza ilimpasa asage kwanza ngano apate unga. Unga ulipokuwa tayari alichanganya na maji ili kutengeneza mikate midogo na kisha akaoka kwenye moto.

40.3 Kisha aliandaa chakula kwa kuuoka mkate huo kwenye moto.

Ghafla akaangalia zile sarafu zake. Alihuzunika sana alipozikuta zikiwa ni tisa tu! Ah, maskini. Mwanamke huyu alikuwa ameiangusha chini sarafu hiyo nyingine.

Alihuzunika sana kwa kuwa moja kati ya sarafu zake azipendazo ilikuwa imepotea. Marafiki zake walimhurumia na wakatumaini kuwa ataipata upesi shilingi yake.

40.4 Ndipo yule mwanamke akainua mkeka na kuangalia chini yake, lakini ile shilingi haikuwepo pale. Alionekana ni mwenye kuhuzunika kwa ajili ya shilingi yake hiyo. Alifagia chumba kizima na akainua taa yake juu ili aone vizuri, hata hivyo hakuweza kuiona shilingi.



Akafagia kona zote za chumba. Ndipo mwisho baada ya kutafuta kwa bidii sana na kwa kufagia, akaiona shilingi, ilikuwa imevingika hadi kwenye kona ya chumba penye giza. Alifurahi sana hata asiweze kuificha furaha yake, akawaita majirani na marafiki zake kwa kuwa ameiona shilingi iliyokuwa imepotea. Akawaabia, **"Furahini pamoja nami, kwa kuwa nimeipata tena ile sarafu iliyopotea."**

40.5 Na sisi tunapokuwa tumetenda dhambi ni kwamba tunakuwa tumepotea kwa Mungu. Jinsi Mungu anavyohuzunika. Lakini tunapomwambia Mungu, kuwa tunaomba msamaha, anakuwa ametupata tena. Jinsi Mungu anavyofurahi anapokuwa ametupata tena. Anafurahia sawana yule mwanamke aliyeipata tena shilingi.